

# “Wenda Wapi (na janga hili) Ewe Ahmad Bâzmûl?!” Sheikh Ahmad an-Najjâr (hafidhahullāh)

28 August, 2015 | Posted by [Salafibayaan](#) | [ClarificationsManhajRefutations](#) | 176 views



Sheikh Ahmad an-Najjâr  
(hafidhahullāh)

## WENDAPI EWE AHMAD BÂZMÛL?!

Katika Mtandao nilipitia kwenye kipande fulani kutoka kwa Ahmad Bâzmûl (hapo awali akijulikana kama ‘al-‘Allâmah’ na baadhi ya vijana, mara ghafla hivi karibuni kama ‘Sheikh’) kwa jina la “Ukosoaji kwa njia ya sauti wa wenye kusema ‘NI KWANINI UNAREJEA KWA SHEIKH RABÎ’ kwa kila kitu?” Basi nikaisikiliza na ikazisisimua nywele zangu mpaka zikasimama wima. Asema ndani yake:

Ni kwanini unafanya marejeo yako kwa Sheikh Rabî’ kwa kila kitu, sisi hatufanyi *ta’assub* kwa Rabî’ [hatumfuati ki-upofu], lakini nataka unipe Mwanachuoni Mkubwa mfano wa Sheikh Rabî’ ambaye naweza kurejea kwake katika wakati wa mitihani, ikhtilafu au fitna! Ama kuhusu mas’ala ya Twahârah na Swalâh, wako ma-‘Ulamâ’ ambao wenye ujuzi na mas’ala hayo ambao naweza kuwarejelea wao, wote wamefanana kwa hayo. Lakini katika mas’ala kwa kina, unahitaji kurejea kwa ma-‘Ulamâ’.

Yâ Allâh, kwa hakika haya ni ya kushangaza mno, ni ukosefu wa adabu wa kiyasi gani huu wa kujificha kwa m-‘Ulamâ’?! Ma-‘Ulamâ hawayafahamu mas’ala ya fitna na mitihani kwahivyo haturudi kwao wakati yakitusibu, ama kuhusiana na Twahârah na Swalâh, basi haya ndiyo mas’ala ya pekee wawezayo kuyafanyia *ijtihâd*?! Eeh Baba Eeh! umewabakishia nini Ahlul-Bid’ah katika kuwatukana ma-‘Ulamâ’?! Hapo awali ilikuwa ikisemwa

kuwahusu ma-‘Ulamâ’ wetu yakwamba “hawafahamu uhakika wa [matukio yanayoendelea]”, kwa maana yakwamba: uhakika wa matukio yanayoendelea yanayoelezwa kwenye magazeti na majarida ya habari, sio uhakika wa kutegemewa. Sasa leo, umefanana nao na unasema “hawajui mas’ala ya *fitan* na *mihan* [fitna na mitihani]”? na kwamba “wao hawaifahamu Manhaj vyema”! Wewe humchi Allâh kwa kuwasababisha vijana kuwakimbia ma-‘Ulamâ’ wao katika mas’ala ya *fitan* na *mihan*? Hebu niambie kwa jina la Mola wako: umeipata kutoka wapi misingi hii ya ufidadi? Wewe wawataka ma-Salafi wawe ni ma-Hizbi?! Wewe wawataka ma-Salafi wasichukuwe chochote isipokuwa kutoka kwa Sheikh mmoja au Mashekhe wachache tu?! Wewe humchi Allâh? Wawachie vijana mambo yao/wao wanataka wafungamanishwe na ma-‘Ulamâ’ wa Ahlus-Sunnah katika mas’ala yote ya dini na imetosha kuwatweza wao. Ikiwa huku sio kumfuata Sheikh Rabî’ ki-upofu, basi ni kupi huko?! Wewe unataka kumtaja kwa jina lisilokuwa lake au vipi?! Amesema Ibn Taymiyyah:

“Yoyote mwenye kufanya *ta’assub* [kumfuata mtu ki-upofu] kwa mtu mmoja makhsusi juu ya wengine, basi yeye ni kama aliyemfanyia *ta’assub* Swahaba mmoja juu ya wengine, kama walivyofanya ma-Râfidhî waliokuwa wakimfanyia *ta’assub* ‘Ali juu ya ma-Khulafâ’ wengine waongofu waliobaki watatu na Maswahaba wengine kwa ujumla; na kama ma-Khawârij waliomtukana ‘Uthmân na ‘Ali. Hizi ni njia za Ahlul-Bid’ah wal-Ahwâ’ ambao imebainishwa katika Kitâb, Sunnah na Ijmâ’ yakwamba walidhibitiwa na kulaumiwa kuwa nje ya mkunjo wa Shari’ah na Manhaj ambayo Allâh aliyomtumiliza nayo Mjumbe (*swallallâhu ‘alayhi wasallam*). Kwahivyo, yoyote atakayekuwa na *ta’assub* kwa mtu mmoja makhsusi anayetokamana na ma-Imâm wa fiqhi atakuwa nafanana na watu hao...”

Mwanachuoni husifiwa jambo fulani, kisha yeye hutoa hukmu yake, na hapana tafauti baina ya sifa inayonasibishwa na mas’ala ya twahâra na sifa inayonasibishwa na mas’ala ya fitna. Labda misingi yako ya ufidadi hapa (Ewe Bâzmûl) ni miovu hata kuwashinda wale wenye kuwalaani ma-‘Ulamâ’ kuwa ati hawaelewei kuhusu *Fiqhul-Wâqi’* kutoka kwenye kipengele kimoja, kwa vile *Wâqi’* si katika Dini na dhana yake ya kutosha haiwezi kufahamika vilivyo ili itolewe hukmu yake, kwahivyo ujinga wao kuhusiana na hilo si udhaifu. Hili ni tafauti na kumtukana ‘Ulamâ’ kwa “kutokuwa na fiqhi ya mas’ala ya *fitna*” na “kutoifahamu Manhaj vilivyo”, kwani makisio ya kutosha ya *fitna* na daraja zake na hukmu zake ni katika Dini na Manhaj vilevile ni katika Dini. Ma-‘Ulamâ’ wana ‘ilmu kuhusu mas’ala ya *fitna* na wala si kama ‘Ulûm ul-Âlah ambayo iliyo na uwezekano wa kubadilika baina ya ma-‘Ulamâ’ na maneno yenyewe yanawahusu ma-‘Ulamâ na wala si walio chini yao.

*Kila sifa njema zinamstahiki Allâh katika hali zote.*

Imeandikwa na,  
Ahmad Muhammad as-Sâdiq an-Najjâr  
Tarehe 24<sup>th</sup> August 2015/10<sup>th</sup> Dhu’l-Qa’dah 1436 AH.  
Kwa mukhtasar kutoka: [http://abuasmaa12.blogspot.com/2015/08/blog-post\\_24.html?spref=tw](http://abuasmaa12.blogspot.com/2015/08/blog-post_24.html?spref=tw)

Imefasiriwa na Abu Farida, Muhammad Awadh Basawad [http://www.qssea.net]

## !!إلى أين يا أحمد بازمول؟

بينما أتصفح الشبكة العنكبوتية وقعت عيني على مقطع لأحمد بازمول ( العلامة سابقا عند بعض الشباب، وشيخ الفجأة لاحقا) بعنوان "رد صوتي على من يقول لماذا كل شيء ترجعون للشيخ ربيع" فسمعتُه فقفتُ شعري منه.

يقول فيه: ( لماذا ترجعون في كل شيء للشيخ ربيع يا أخي نحن ما نتعصب لربيع، لكن انتني بعالم كبير مثل الشيخ ربيع أنا أذهب إليه عند الخن والخلافات والفتن أما مسائل الطهارة والصلاة يحسنها العلماء أرجع إليهم كلهم عادي

لكن في مسائل دقيقة تحتاج الرجوع الى العلماء ) يا لله العجب ما هذا الطعن المبطن في العلماء؟! أمور الفتن والخن لا يدركها العلماء فلا يرجع إليهم فيها، أما الطهارة والصلاة فهذا هو محل اجتهادهم!. يا رجل ماذا تركت لأهل البدع من الطعن في علمائنا؟! قديما قيل فيهم: لا يفقهون الواقع( اي واقع الجرائد ونشرات الأخبار لا الواقع الذي يتوقف عليه التصور) واليوم شابتهم فقلت فيهم: لا يعرفون أمور الفتن والخن!! ولا يحسنون المنهج!

ألا تخاف من الله في تنفير الشباب عن علمائهم في أمور الفتن والخن؟! قل لي بربك من أين تستقي هذه التأصيلات الفاسدة؟! أتريد من السلفيين أن يكونوا حزبيين؟! أتريد من السلفيين ألا يصدرُوا إلا عن شيخ واحد أو بعض الشيوخ؟!

ألا تتق الله

دَعِ الشَّابَّ وَشَأْنَهُمْ

يرتبطون بعلماء أهل السنة في الدين كله.

وكفالك تنقصا لهم.

إن لم يكن هذا تعصبا للشيخ ربيع فماذا يكون إذن؟

أتريد أن تسميه بغير اسمه أو ماذا؟!

قال ابن تيمية:(ومن تعصب لواحد بعينه من الأئمة دون الباقي فعو بمنزلة من تعصب لواحد بعينه من الصحابة دون الباقي، كالرافضي الذي يتعصب لعلي دون الخلفاء الثلاثة وجمهور الصحابة، وكالخارجي الذي يقدح في عثمان وعلي فهذه طرق أهل البدع والأهواء الذين ثبت بالكتاب والسنة والإجماع أنهم مذمومون خارجون عن الشريعة والمنهاج الذي بعث الله به رسوله ﷺ. فمن تعصب لواحد بعينه من الأئمة ففيه شبهة من هؤلاء...)

والعالم ينقل له الوصف فيبين الحكم، فلا فرق بين وصف متعلق بالطهارة أو وصف متعلق بالفتن.

يا رجل لربما بتأصيلك الفاسد هذا تكون أشد ممن لزوا العلماء بعدم فقه الواقع من جهة أن الواقع ليس من الدين ولا يتوقف عليه تصور الحكم، فجهلهم به ليس فيه منقصة  
بخلاف أن يلمزوا بعدم فقههم لباب الفتن، وعدم إحسانهم للمنهج.  
وإعطاء الفتنة قدرها ومنزلتها وحكمها من الدين.  
والمنهج من الدين.

وأمر الفتن يشترك بعلمها العلماء في الجملة  
وليس هي كعلوم الآلة التي ربما يتفاوت في بعضها العلماء.  
والكلام عن العلماء لا فيمن دونهم.  
والحمد لله على كل حال.

وكتبه

أحمد محمد الصادق النجار

م 12:05 في أحمد الصادق مرسله بواسطة

Salafibayaan allows for this article in its present form and with no alterations to be distributed, printed photocopied and disbursed by electronic means for the purpose of spreading its content with the condition that the link is given to this article and the publisher is acknowledged.